

## **Mradi Namba 4279: UPANUZI WA USIKIVU KWA SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)**

Kwa mwaka 2022/23 **Sh. 13,136,500,000** ziliombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mradi tajwa. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Upanuzi wa Usikivu redio za TBC kwenye maeneo yasiyokuwa na ausikivu nchini;
- (ii) Ukarabati wa ofisi, ununuzi wa Mitambo na vifaa vya utangazaji vya Chaneli ya Tanzania Safari;
- (iii) Kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook);
- (iv) Kuwezesha ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);
- (v) Ujenzi jengo la Makao Makuu ya TBC Dodoma na ukarabati wa majengo ya Ofisi yaliyopo;
- (vi) Kuwezesha ununuzi wa Magari ya kurushia matangazo mubashara ya Redio (TBC Taifa na TBC FM) na Televisheni (TBC1, TB2 na TBC Online) na pia Magari kwa ajili ya Shughuli nyingine za Utangazaji;
- (vii) Kuwezesha ununuzi wa vifaa 18 vya kurushia Matangazo mubashara ya Redio nje ya studio;
- (viii) Ununuzi wa mitambo 10 na vifaa vya kurushia matangazo mubashara ya Televisheni (TBC1, TBC2 na Ofisi za Kanda);
- (ix) Ukarabati, uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi wa Nchi Kusini mwa Afrika katika jengo la utangazaji Barabara ya Nyerere kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya picha na sauti;
- (x) Ufungaji wa mifumo ya uhariri, upokeaji na urushaji wa Matangazo kupitia mifumo ya TEHAMA (Robotic Intergrated News system with international news Monitoring); na
- (xi) Kuwezesha ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBC Mtandaoni na televisheni ya Kiingereza ya online.

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2022 Wizara ilipokea jumla ya Sh **1,952,529,729.09** sawa na asilimia **14.9** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

- (i) Taratibu za manunuzi zimeshakamilika na wazabuni wameshapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Upanuzi wa Usikivu redio za TBC katika maeneo 9 (Kalambo – Rukwa, Liwale – Lindi, Rufiji – Pwani, Kakonko – Kigoma, Mfundu – Iringa, Kaliua – Tabora, Igunga – Tabora, Manyoni – Singida na Karatu –

Manyara). Aidha, Mikataba yote inatarajiwa kusainiwa ifikapo mwezi Februari, 2023

- (ii) Upembuzi yakinifu wa michoro na mifumo kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Kituo cha Taifa cha Televisheni (TVT) - Mikocheni Dar Es Salaam litakalotumika kwa ajili ya Chaneli ya Utalii na utawala zinaendelea na zinatarajia kukamilika mwezi Januari, 2023.
- (iii) Kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya Kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook) – awamu ya pili, mkataba unatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa mwezi Januari, 2023.
- (iv) Taratibu za manunuzi ya mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring) zimekamilika
- (v) Vibali kwa ajili ya ununuzi wa magari kwa ajili ya shughuli za utangazaji vimeshapatikana toka Ofisi ya Waziri Mkuu. TBC inasubiri gharama za magari hayo toka GPSA kwa ajili ya utekelezaji. Maombi ya Fedha za ununuzi wa magari haya yatawasilishwa Hazina mwezi Januari, 2023.
- (vi) Taratibu za Ununuzi wa vifaa vya kurushia Matangazo mbashara ya Redio, televisheni na mitandao ya kijamii nje ya studio zimeshakamilika. TBC imeshawalisha maombi ya fedha Hazina kiasi cha **Sh. 656,000,000**;
- (vii) Maombi ya fedha kwa ajili ya Ukarabati wa studio za redio (Awamu ya Pili), uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya picha na Sauti kiasi cha **Sh. 1,357,019,322.02** yameshawalishwa Hazina tangu mwezi Novemba, 2022 baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi na mzabuni kupatikana. Ukarabati utanza mara baada ya kupatikana kwa fedha;
- (viii) Taratibu za Ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBCMtandaoni na televisheni ya Kiingereza ya online zimeshakamilika na fedha zimeshaombwa Hazina; na
- (ix) Mzabuni kwa ajili ya Ufungaji wa Mitambo ya redio na TEHAMA katika studio za redio barabara ya Nyerere pamoja na jengo la TBC2 awamu ya pili ameshapatikana baada ya kukamilika kwa taratibu za manunuzi. Mkataba umewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya mapitio. Utekelezaji unatarajia kuanza Februari, 2023.